**MULIKA Na. 40(2) 2021 (1-22)**

# Mikabala ya Uchanganuzi wa Viambajengo vya Sentensi na Istilahi Zinazotumika: Mifano kutoka Lugha ya Kiswahili

*Fabiola Hassan*[1]

**Chuo Kikuu cha Dodoma**

## Ikisiri

Uchanganuzi wa viambajengo vya sentensi unaweza kufanywa kwa kutumia mikabala mbalimbali. Kila mkabala unaambatana na matumizi ya istilahi zake mahususi. Licha ya kuwapo kwa mipaka ya istilahi hizo, bado kuna uchanganyaji wa matumizi yake. Uchanganyaji huu unaashiria kwamba mikabala ya uchanganuzi wa viambajengo vya sentensi na istilahi zinazohusika ni masuala ambayo hayako wazi sana miongoni mwa wanaisimu. Hivyo, makala haya yanahusu mikabala ya uchanganuzi wa viambajengo vya sentensi na istilahi zinazohusika kwa kutumia mifano kutoka lugha ya Kiswahili. Data za makala haya zimepatikana kwa njia ya hojaji, usaili na uchambuzi matini. Ufafanuzi wa data umeongozwa na misingi ya Nadharia ya Sarufi Leksia Amilifu ya Bresnan na Kaplan (ya mwishoni mwa miaka ya 1970). Matokeo yanaonesha kwamba viambajengo vya sentensi vinaweza kuchanganuliwa kimuundo, kiuamilifu, kisemantiki na kipragmatiki. Kwa kuzingatia mikabala hii, kuna istilahi za kimuundo, kiuamilifu, kisemantiki na kipragmatiki. Kwa ujumla, makala haya yanahitimisha kwamba istilahi za uchanganuzi wa viambajengo vya sentensi hazitumiki kiholela, bali huamuliwa na mikabala ya uchanganuzi wa viambajengo.

## 1.0 Utangulizi

Viambajengo vya sentensi vinaweza kuchanganuliwa kimuundo, kiuamilifu, kisemantiki na kipragmatiki. Kila mkabala unatumia istilahi zinazotambulisha viambajengo vya sentensi. Kwa kuwa mikabala ni tofauti, ni dhahiri kuwa istilahi zinatofautiana kutoka mkabala mmoja hadi mwingine. Hata hivyo, pamoja na kuwapo kwa tofauti bayana, bado kuna uchanganyaji wa matumizi ya istilahi katika changanuzi mbalimbali zinazofanywa na wanaisimu. Kwa mfano, Phillipo (2018) akifafanua uchanganuzi wa Wanamapokeo, anaeleza kuwa sentensi, *Rehema atapika ubwabwa leo* inachanganuliwa kama ifuatavyo: neno *Rehema* ni Nomino (N), *atapika* ni Kitenzi (T), *ubwabwa* ni Shamirisho (Sh) na *leo* ni Chagizo (Ch).

[1] **Baruapepe:** *fabiola.hassan@udom.ac.tz*

Uchanganuzi huu umetumia istilahi za kimuundo nomino na kitenzi. Pia, umetumia istilahi za kiuamilifu shamirisho na chagizo. Hii inaonesha kwamba kuna uchanganyaji wa matumizi ya istilahi. Uchanganyaji huu unatokana na kukosa uelewa wa kutosha juu ya matumizi ya istilahi za uchanganuzi wa viambajego. Uchanganyaji wa matumizi ya istilahi unazalisha tatizo la kushindwa kuweka mpaka baina ya mikabala mbalimbali ya uchanganuzi. Kutokana na tatizo hilo, uchanganuzi wa viambajengo unaonekana kuwa ni mchakato mgumu, holela na usiofuata kanuni. Makala haya yanahusu matumizi ya istilahi katika uchanganuzi wa viambajengo vya sentensi kwa kutumia mifano ya Kiswahili. Ili kufikia lengo hili, makala yanafafanua mikabala ya uchanganuzi wa viambajengo vya sentensi na istilahi zinazohusika katika kila mkabala. Makala haya yana sehemu tano ikiwa ni pamoja na sehemu hii ya utangulizi. Sehemu ya pili inahusu mbinu zilizotumika katika kukusanya data. Sehemu ya tatu ni ufafanuzi wa Nadharia ya Sarufi Leksia Amilifu. Sehemu ya nne inafafanua mikabala na istilahi zinazotumika katika uchanganuzi wa viambajengo vya sentensi katika Kiswahili. Sehemu ya tano inatoa hitimisho la jumla la makala haya. Baada ya utangulizi huu, sehemu inayofuata inahusu ufafanuzi wa mbinu zilizotumika kukusanya data.

## 2.0 Mbinu Zilizotumika Kukusanya Data

Data za makala haya zimepatikana kwa mbinu ya hojaji, usaili na uchambuzi wa matini. Mbinu ya hojaji ilihusisha jumla ya wanafunzi wanne (4) wa shahada za umahiri na uzamivu katika Kiswahili, wawili (2) kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na wawili (2) kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Wanafunzi hao walipewa hojaji yenye sentensi zilizohitaji kuchanganuliwa kimuundo, kiuamilifu, kisemantiki na kimawasiliano. Mbinu ya usaili ilitumika kukusanya data kutoka kwa wahadhiri wanne (4) wa Sintaksia ya Kiswahili, wawili (2) kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na wawili (2) kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Mtafiti alitumia mwongozo wa usaili uliokuwa na maswali kuhusu mikabala na istilahi za uchanganuzi wa viambajengo. Uchambuzi wa matini ulihusisha vitabu 4 vinavyohusu sintaksia ya Kiswahili. Vitabu hivyo ni *Utangulizi wa Lugha na Isimu* (Besha, 1994), *Kozi Tangulizi katika Sarufi Miundo ya Kiswahili* (Wessana-Chomi, 2003), Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (Massamba, Kihore na Hokororo, 2000) pamoja na *Sintaksia ya Kiswahili: Nadharia za Kisintaksia na Uchanganuzi wa Kiswahili* (Phillipo na Kuyenga, 2018). Mtafiti alisoma mada zinazohusu uchanganuzi wa viambajengo huku akibainisha mikabala na istilahi zinazotumika.

## 3.0 Nadharia ya Sarufi Leksia Amilifu

Uchambuzi na ufafanuzi wa data zilizotumika umeongozwa na Nadharia ya Sarufi Leksia Amilifu (SLA). SLA ni nadharia iliyoasisiwa na Joan Bresnan na Ronald Kaplan mwishoni mwa miaka ya 1970. Nadharia hii inahusu ufafanuzi wa lugha kwa kutumia taarifa za kileksika na uamilifu wa viambajengo vya sentensi. Nadharia hii inahusisha matumizi ya mikabala katika uchanganuzi wa viambajengo. Mikabala hiyo ni Mkabala wa Miundo ya Viambajengo, Mkabala wa Uamilifu wa Viambajengo, Mkabala wa Vishiriki vya Kitenzi na Mkabala wa Muundo Taarifa. Mkabala wa Miundo ya Viambajengo unahusu miundo ya viambajengo. Mkabala huu unaonesha maneno, virai na mfuatano wake katika

sentensi. Mkabala huu umesaidia kuonesha uchanganuzi wa viambajengo kimuundo na istilahi zinazohusiana na viambajengo hivyo. Mkabala wa Uamilifu wa Viambajengo unahusu uamilifu wa viambajengo. Mkabala huu unaonesha dhima za kisarufi za viambajengo. Dhima hizo ni kiima, yambwa, yambiwa, yambwa$_{\theta}$, oblikyu$_{\theta}$[2], kijalizo na chagizo. Mkabala huu umesaidia kufafanua uchanganuzi wa viambajengo kiuamilifu na istilahi zinazowakilisha viambajengo hivyo. Mkabala wa Vishiriki vya Kitenzi unahusu vishiriki vya kitenzi. Mkabala huu unaonesha idadi na dhima za kisemantiki za vishiriki vya kitenzi kinachotumika kuunda sentensi. Mathalani, kitenzi *weka* kinahitaji mwekaji (mtenda), kinachowekwa (kithimu), na mahali (kimahali). Mkabala huu umesaidia kufafanua uchanganuzi wa viambajengo kisemantiki na istilahi zinazohusiana na viambajengo hivyo. Mkabala wa Muundo wa Taarifa, kipragmatiki (kimawasiliano), unaonesha aina na mpangilio wa taarifa katika sentensi. Unaeleza kwamba, sentensi ina taarifa inayofahamika (mada) na taarifa mpya (fokasi). Taarifa hizi zinawakilishwa na viambajengo. Mkabala huu umefafanua uchanganuzi wa viambajengo na istilahi zinazotumika. Kwa ujumla, Nadharia ya SLA imetumika kubainisha mikabala na istilahi za uchanganuzi wa viambajengo vya sentensi.

## 4.0 **Mikabala na Istilahi za Uchanganuzi wa Viambajengo vya Sentensi katika Lugha ya Kiswahili**

Viambajengo vya sentensi za Kiswahili vinaweza kuchanganuliwa kwa kutumia mikabala minne. Mikabala hiyo ni Mkabala wa Miundo ya Viambajengo, Mkabala wa Uamilifu wa Viambajengo, Mkabala wa Vishiriki vya Kitenzi na Mkabala wa Muundo wa Taarifa. Kila mkabala unatumia istilahi mbalimbali kuwakilisha viambajengo. Sehemu zinazofuata zinafafanua mikabala hiyo na istilahi zinazotumika.


### 4.1 Mkabala wa Miundo ya Viambajengo

Mkabala huu unachanganua viambajengo kwa kutumia miundo ya viambajengo. Mkabala huu unaonesha maneno na virai vinavyounda sentensi. Unaeleza kwamba sentensi ina sehemu kuu mbili, yaani kirai nomino (KN) na kirai kitenzi (KT). Virai hivi vinaweza kuundwa na virai vingine. Virai hivyo ni kirai nomino, kirai kitenzi, kirai kivumishi, kirai kielezi na kirai kihusishi. Pia, kirai kinaundwa na maneno mbalimbali. Maneno hayo ni nomino (N), kitenzi (T), kivumishi (V), kielezi (E) na kihusishi (H). Kielelezo Na. 1 kinaonesha uchanganuzi wa viambajengo vya sentensi kimuundo:

.

[2]Alama $_{\theta}$ **inamaanisha** kwamba dhima ya kisarufi inayohusika inahusishwa na dhima mahususi za kisemantiki.

*Mtoto mdogo anakula chakula.*




***Kielelezo Na. 1: Miundo ya Viambajengo***

Kielelezo Na. 1 kinaonesha miundo ya viambajengo vya sentensi *Mtoto mdogo anakula chakula*. Sentensi hii ina $KN_1$ (*mtoto mdogo*), KT (*anakula chakula*), KV (*mdogo*) na $KN_2$ (*chakula*). Pia, kuna maneno $N_1$ (*mtoto*), V (*mdogo*), T (*anakula*) na $N_2$ (*chakula*). Hivyo, S imeundwa na $KN_1$ na KT. Aidha, $KN_1$ kimeundwa na $N_1$ na KV; KV kimeundwa na V. KT kimeundwa na T na $KN_2$, na $KN_2$ kimeundwa na $N_2$. Kwa ujumla, virai na maneno haya ni viambajengo vya sentensi *Mtoto anakula chakula*.

### 4.1.1 Istilahi za Kimuundo

Uchanganuzi wa viambajengo kimuundo unatumia istilahi za kimuundo kuanzia ngazi ya neno, kirai, kishazi[3] na sentensi. Zifuatazo ni istilahi zinazotumika katika Kiswahili:

**(a) Sentensi**

Kimuundo, sentensi ni tungo ya juu ambayo inaundwa na kishazi kimoja au zaidi. Kwa kuzingatia aina za sentensi kimuundo, kuna istilahi zinazoonesha muundo wa sentensi. Istilahi hizo ni hizi zifuatazo:

Mosi, *sentensi sahili*. Hii ni sentensi ambayo imeundwa na kishazi huru. Mifano Na. 1 (a) na 1 (b) inaonesha sentensi sahili za Kiswahili:

1. Sentensi sahili
a) Mwalimu anafundisha Kiswahili.
b) Mwanafunzi anasoma kitabu.

Mifano Na. 1 (a) na 1 (b) inaonesha sentensi sahili. Sentensi hizi zimeundwa na kishazi huru kimojakimoja tu. Hivyo, *sentensi sahili* ni istilahi ya kimuundo.

---

[3] Tungo kishazi haijidhihirishi waziwazi katika uchanganuzi wa viambajengo kimuundo. Licha ya kufanya hivyo, tungo hii ina istilahi zake ambazo zinatumika kidhahania.

Pili, *sentensi changamani*. Hii ni sentensi ambayo imeundwa na viambajengo viwili ambavyo ni kishazi huru na kishazi tegemezi. Mifano Na. 2 (a) na 2 (b) inaonesha sentensi changamani za Kiswahili:

2. Sentensi Changamani
a) Mwalimu anayefundisha Kiswahili ni mpole sana.
b) Mwanafunzi anayeingia darasani amefaulu mtihani.

Mifano Na. 2 (a) na 2 (b) inaonesha sentensi changamani. Sentensi hizi zimeundwa na viambajengo viwiliviwili. Kiambajengo cha kwanza ni kishazi tegemezi; *Mwalimu anayefundisha Kiswahili* na *Mwanafunzi anayeingia darasani*, mtawalia. Kiambajengo cha pili ni kishazi huru; *Mwalimu ni mpole sana* na *Mwanafunzi amefaulu mtihani*, mtawalia. Hivyo, *sentensi changamani* ni istilahi ya kimuundo.

Tatu, *sentensi ambatani*. Hii ni sentensi inayoonesha kwamba sentensi imeundwa na viambajengo viwili au zaidi. Viambajengo hivyo vinaweza kuwa sentensi sahili peke yake, changamani peke yake au sahili na changamani. Mifano Na. 3 (a) na (b) inaonesha sentensi ambatani katika Kiswahili:

3. Sentensi ambatani
a) Baba analima shamba na mama anapika chakula.
b) Mwalimu anayeingia darasani anafundisha Kiswahili na mwalimu aliyeondoka darasani anaandika.

Mifano Na. 3 (a) na 3 (b) inaonesha sentensi ambatani. Sentensi hizi zimeundwa na viambajengo viwiliviwili. Mfano wa (3a) umeundwa na sentensi sahili mbili, yaani *Baba analima shamba* na *mama anapika chakula*. Mfano wa (3b) umeundwa na sentensi changamani mbili, yaani *Mwalimu anayeingia darasani anafundisha Kiswahili* na *Mwalimu aliyeondoka darasani anafundisha Kiingereza*. Hivyo, *sentensi ambatani* ni istilahi ya kimuundo.

Hivyo, tunapotumia istilahi hizi; yaani, sentensi sahili, sentensi changamani na sentensi ambatani, tunarejelea istilahi za kimuundo na kwamba, tunaifafanua sentensi kwa kutumia mkabala wa kimuundo.

**(b) Kishazi**
Hii ni istilahi inayorejelea muundo wa kiambajengo. Kishazi ni tungo iliyoundwa na muunganiko wa virai viwili ama zaidi. Istilahi hii inaonesha muundo wa kiambajengo cha tungo. Kwa kuzingatia muundo wa kishazi, tunapata istilahi mbili.

Mosi, ni *kishazi huru*. Hiki ni kishazi kilichojitosheleza kimuundo. Kishazi hiki hakihitaji kiambajengo kingine ili kujitosheleza kimuundo na kimaana. Mifano Na. 4 (a) na 4 (b) inaonesha vishazi huru vya Kiswahili:

4. Vishazi Huru
a) Mama anafua nguo.
b) Mtoto anapiga mpira.

Mifano Na. 4 (a) na 4 (b) inaonesha vishazi huru *Mama anafua nguo* na *Mtoto anapiga mpira*, mtawalia. Vishazi hivi vimejitosheleza kimuundo na kimaana. Kwa hiyo, istilahi *kishazi huru* ni ya kimuundo kwa sababu inaashiria muundo wa kiambajengo.

Pili, ni *kishazi tegemezi*. Hiki ni kishazi kisichojitosheleza kimuundo na, kwamba, kinahitaji kiambajengo kingine ili kujikamilisha kimuundo na kimaana. Mifano Na. 5 (a) na 5 (b) inaonesha vishazi tegemezi vya Kiswahili:

5. Vishazi Tegemezi
a) Mtoto aliyeingia darasani
b) Mtoto aliyeingia dasani amefaulu mtihani.
c) Mwalimu anayefundisha Kiswahili
d) Mwalimu anayefundisha Kiswahili anawapenda wanafunzi wake.

Mfano Na. 5 (a) na 5 (c) inaonesha vishazi tegemezi *Mtoto aliyeingia darasani* na *mwalimu anayefundisha Kiswahili*, mtawalia. Vishazi hivi havijitoshelezi na, hivyo, vinahitaji viambajengo vingine ili kujikamilisha kimuundo na kimaana. Kwa hiyo, vishazi hivi vikiambatana na viambajengo vingine hujitosheleza kimuundo na kimaana kama inavyoonekana katika mifano Na. 5 (b) na 5 (d). Kwa hiyo, *kishazi huru* na *kishazi tegemezi* ni istilahi za kimuundo.

**(c) Kirai**
Hii ni istilahi inayorejelea muundo wa tungo. Istilahi hii inarejelea tungo iliyoundwa na neno moja au zaidi. Kimuundo, kirai kinaundwa na neno kuu peke yake au neno kuu na kijalizi. Kwa kuzingatia uainishaji wa virai kimuundo, kuna istilahi zinazotumika katika uchanganuzi wa viambajengo vya sentensi.

Mosi, **ni** *Kirai Nomino (KN).* Hii ni istilahi inayorejelea kirai kilichoundwa na nomino peke yake kama neno kuu au nomino kama neno kuu na maneno mengine kama kijalizi. Mifano Na. 6 (a) na 6 (b) inaonesha kirai nomino katika Kiswahili:
6. Virai Nomino
a) <u>Mzee</u> anatembea vizuri.
KN
b) <u>Mtoto</u> anakula <u>chakula kitamu</u>.
KN KN

Mfano Na. 6 (a) unaonesha KN mzee katika sentensi ya Kiswahili. Kirai hiki kimeundwa na neno kuu ambalo ni nomino *mzee* peke yake. Mfano Na. 6 (b) unaonesha KN *chakula kitamu* katika sentensi ya Kiswahili. Kirai hiki kimeundwa na neno kuu *chakula* na kijalizo *kitamu*. Hivyo, *kirai nomino* ni istilahi ya

kimuundo.

Pili, **ni** *Kirai Kitenzi (KT).* Hii ni istilahi inayorejelea kirai kilichoundwa na kitenzi peke yake kama neno kuu au kitenzi kama neno kuu pamoja na neno au maneno mengine kama viijalizo vya kitenzi. Mifano Na. 7 (a) na (b) inaonesha virai vitenzi katika Kiswahili:

7. Kirai Kitenzi

a) Mzee anatembea.
KT

b) Mtoto anakula chakula kitamu.
KT

Mfano Na. 7 (a) unaonesha KT *anatembea* katika sentensi ya Kiswahili. Kirai hiki kimeundwa na neno kuu ambalo ni kitenzi *anatembea* peke yake. Mfano Na. 7 (b) unaonesha KT *anakula chakula*. Kirai hiki kimeundwa na neno kuu ambalo ni kitenzi *anakula* na kijalizo *chakula.* Hivyo, *kirai kitenzi* ni istilahi ya kimuundo.

Tatu, ni *Kirai Kivumishi (KV).* Hii ni istilahi inayorejelea kirai kilichoundwa na kivumishi peke yake kama neno kuu au kivumishi kama neno kuu pamoja na maneno mengine kama kijalizo. Mifano Na. 8 (a) na (b) inaonesha virai vivumishi vya Kiswahili:

8. Kirai Kivumishi

a) Mzee mfupi anatembea vizuri.
KV

b) Mtoto mchafu sana anakula chakula kitamu.
KV

Mfano Na. 8 (a) unaonesha KV *mfupi* katika sentensi. Kirai hiki kimeundwa na neno kuu ambalo ni kivumishi *mfupi* pekee. Mfano Na. 8 (b) unaonesha KV *mchafu sana* katika sentensi. Kirai hiki kimeundwa na neno kuu ambalo ni kivumishi *mchafu* na kijalizo *sana*. Hivyo, *kirai kivumishi* ni istilahi ya kimuundo.

Pia, kuna *Kirai Kielezi (KE).* Hii ni istilahi inayorejelea kirai kilichoundwa na kielezi pekee kama neno kuu au kielezi kama neno kuu na maneno mengine kama kijalizo. Mifano Na. 9 (a) na 9 (b) inaonesha virai vielezi katika Kiswahili:

9. Kirai Kielezi

a) Mzee anatembea vizuri.
KE

b) Mtoto anakula vizuri sana.
KE

Mfano Na. 9 (a) unaonesha KE *vizuri* katika sentensi. Kirai hiki kimeundwa na neno kuu ambalo ni kielezi *vizuri* pekee. Mfano Na. 9 (b) unaonesha KE *vizuri sana* katika sentensi. Kirai hiki kimeundwa na neno kuu ambalo ni kielezi *vizuri* na kijalizo *sana* ambacho ni kielezi. Hivyo, *kirai kielezi* ni istilahi ya kimuundo.

Aidha, kuna *Kirai Kihusishi (KH).* Hii ni istilahi inayorejelea kirai kilichoundwa

na kihusishi kama neno kuu na maneno mengine kama kijalizo. Mifano Na. 10 (a) na 10 (b) inaonesha virai vihusishi katika Kiswahili:

10. Kirai Kihusishi
a) Mzee wa busara anatembea vizuri.
b) Mtoto anakula chakula cha mama.

Mifano Na. 10 (a) na 10 (b) inaonesha KH *wa busara* na *cha mama*, mtawalia. Virai hivi vimeundwa na maneno makuu ambayo ni vihusishi *wa* na *cha*, mtawalia. Pia, vimeundwa na vijalizo *busara* na *mama*, mtawalia. Hivyo, kirai kihusishi ni istilahi ya kimuundo.

**(d) Istilahi Zinazotaja Kategoria za Maneno**

Licha ya istilahi zinazohusu virai, vishazi na sentensi; pia, zipo istilahi za kimuundo zinazotaja kategoria za maneno. Licha ya kuwapo kwa kategoria mbalimbali za maneno, tumefafanua istilahi zinazorejelea kategoria kuu zinazounda virai katika Kiswahili. Hivyo, istilahi ya kwanza ni *Nomino (N)*. Hili ni neno ambalo linalotaja mtu, kitu, hali, mahali au kiumbe. Kimofolojia, ni neno linaloweza kupokea viambishi vya ngeli na idadi. Kisintaksia ni neno linalotokea katika nafasi ya kiima, yambwa, yambiwa, kijalizo, au chagizo. Neno hili mara nyingi hufuatwa na kivumishi katika tungo. Nomino ni neno linalounda neno kuu katika kirai nomino. Mifano ya nomino ni *baba*, *mama*, *mtoto*, *msichana* na *mwalimu*. Hivyo, *nomino* ni istilahi ya kiuambajengo katika lugha.

Istilahi ya pili ni *Kitenzi (T)*. Hili neno ambalo linataja tendo lililotendeka, linalotendeka, au litakalotendeka. Kimofolojia, ni neno linaloweza kupokea viambishi vya upatanishi wa kisarufi, njeo, hali, urejeshi, ujirejeshi, yambwa, yambuzi, tamati na viangami. Kisintaksia ni neno linalotokea baada ya kiima katika mfuatano wa kawaida wa vipashio. Neno hili mara nyingi hufuatwa na yambwa katika tungo. Kitenzi ni neno linalounda neno kuu katika kirai kitenzi. Mifano ya vitenzi ni *analima*, *anasoma*, *anakula* na *anaingia*. Hivyo, *kitenzi* ni istilahi ya kiuambajengo katika lugha.

Istilahi nyingine ni *Kivumishi (V)*. Kivumishi ni neno ambalo linakumusha nomino au kiwakilishi chake. Kimofolojia, ni neno linaloweza kupokea viambishi vya upatanishi katika kirai nomino. Aidha, kisintaksia ni neno linalotokea baada ya nomino au kiwakilishi chake. Kimsingi, kivumishi ni neno linalounda neno kuu katika kirai kivumishi. Mifano ya vivumishi katika lugha ya Kiswahili ni *mrefu*, *mpole*, *mdogo* na *mweusi*. Hivyo, *kivumishi* ni istilahi ya kiuambajengo katika lugha.

Pia, kuna *Kielezi (E)*. Hii ni istilahi inayorejelea neno linalotoa taarifa zaidi kuhusu kitenzi. Hueleza tendo lilifanyika wapi, lini, wakati gani, au kwa namna gani. Kimofolojia, ni neno linaloweza kupokea kiambishi cha kisarufi. Kisintaksia ni neno linalotokea baada ya kitenzi. Kielezi ni neno linalounda neno kuu katika kirai kielezi. Mifano ya vielezi katika lugha ya Kiswahili ni *polepole*, *kidogo*, *sana* na

*haraka*. Hivyo, *kielezi* ni istilahi ya kiuambajengo katika lugha.

Aidha, kuna *Kihusishi* (H). Istilahi hii inarejelea neno linalohusianisha neno moja na jingine, mathalani nomino na nomino. Kimofolojia, hili ni neno linalopokea kiambishi cha upatanishi neno linalohusishwa. Aidha, kisintaksia ni neno linalotokea baada ya kitenzi, nomino, au kiwakilishi. Kwa upande mwingine, kihusishi hutokea kabla ya nomino. Kimsingi, kihusishi, ni neno linalounda neno kuu katika kirai kihusishi. Mifano ya vihusishi katika Kiswahili ni *wa*, *ya*, *za* na *la*. Hivyo, *kihusishi* ni istilahi ya kiuambajengo katika lugha.

Kwa ujumla, katika sehemu hii, tumefafanua Mkabala wa Miundo ya Viambajengo na baadhi ya istilahi zinazotumika katika kuchanganua viambajengo vya sentensi. Mkabala huu ni faafu kwa sababu unaonesha uambajengo wa sentensi, yaani namna gani viambajengo vya chini vinaungana kuunda kiambajengo cha juu zaidi. Mkabala huu umeonesha ni kwa namna gani unaweza kuchanganua viambajengo vya sentensi kimuundo kwa kutumia istilahi za kimuundo. Kwa kuzingatia data zilizotolewa na watoataarifa katika changanuzi walizozifanya, mkabala huu unaondoa changamoto ya kuchanganya matumizi ya istilahi za kimuundo na za mikabala mingine kama tulivyoeleza katika sehemu ya utangulizi. Hata hivyo, licha ya ufafanuzi huu nzuri, mkabala huu hauoneshi uamilifu wa viambajengo na muundo wa taarifa unaowakilishwa na viambajengo vinavyounda tungo inayohusika. Kwa kuwa mkabala huu una mapungufu, uchanganuzi wa viambajengo vya sentensi unaweza kufanywa kwa kutumia mikabala mingine. Sehemu 4.2 inafafanua Mkabala wa Uamilifu wa Viambajengo.

### 4.2 Mkabala wa Uamilifu wa Viambajengo

Huu ni mkabala unaozingatia uamilifu wa viambajengo. Katika mkabala huu, uchanganuzi wa sentensi unazingatia dhima (uamilifu) za kisarufi za viambajengo vya sentensi[4]. Dhima hizo ni kama vile kiima, yambwa, yambiwa, yambwa$_{\theta}$, oblikyu$_{\theta}$, kijalizo na chagizo. Dhima hizi zinaashiriwa na sifa za kimofosintaksia za viambajengo vinavyohusika. Mfano wa sifa hizo ni ngeli, uyambwa, upatanishi wa kisarufi na urejeshi. Kielelezo Na. 2 kinaonesha uchanganuzi wa viambajengo kiuamilifu:

[4] Katika makala haya istilahi dhima za kisarufi imetumika kurejelea uamilifu wa kisarufi unaofanywa na viambajengo vya sentensi.

*Mtoto mdogo anakula chakula.*

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kiima | PRED | Mtoto mdogo | |
| | kng1 | = | m |
| Kitenzi | Anakula | | |
| | kk1 | = | a |
| | knj | = | na |
| | ksuk | = | ku |
| Yambwa | PRED | | chakula |
| | kng7 | = | ch |

***Kielelezo Na. 2: Uamilifu wa Viambajengo vya Sentensi***

Kielelezo Na. 2 kinaonesha dhima za kisarufi za viambajengo vya sentensi *Mtoto mdogo anakula chakula*. Dhima hizo ni kiima (*mtoto mdogo*) na yambwa (*chakula*). Pia, kinaonesha sifa za kimofosintaksia za viambajengo vya sentensi. Sifa hizo zinawakilishwa na kiambishi ngeli ya 1, yaani kk1 {*m*-}, kipatanishi kiima 1, yaani kk1 {*a*-}, kiambishi njeo, yaani knj {-*na*-}, kiambishi siukomo, yaani ksuk {-*ku*-} pamoja na kiambishi ngeli ya 7, yaani kng 7 {*ch*-}. Kwa hiyo, uchanganuzi wa viambajengo vya sentensi unaweza kufanywa kwa kutumia Mkabala wa Uamilifu wa Viambajengo.

### 4.2.1 Istilahi za Kiuamilifu za Viambajengo vya Sentensi

Hizi ni istilahi zinazohusiana na dhima za viambajengo katika sentensi. Istilahi hizo zinaonesha mahusiano ya kisarufi baina ya kiambajengo kimoja na kingine katika sentensi. Zifuatazo ni istilahi zinazohusiana na uamilifu wa viambajengo vya sentensi.

#### (a) Kiima

Kiima ni istilahi inayoonesha dhima ya kisarufi ya kiambajengo katika sentensi. Wanaisimu mbalimbali wamefafanua sifa za kiima (taz. Keenan, 1976a; TUKI, 1990; Van Valin, 2001; Mkude, 2005). Kiima kina sifa zifuatazo: kwanza, katika sentensi yenye mpangilio wa kawaida, kiima kinatokea mwanzoni mwa sentensi kabla ya kitenzi. Pili, kiima kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi kwa kutumia kiambishi cha upatanishi wa kiima. Tatu, kiima kinaweza kurejeshwa na kuwakilishwa na kiambishi cha urejeshi katika kitenzi. Vilevile, kiima kinawakilisha taarifa ambayo ni mada katika sentensi. Hata hivyo, kiambajengo ambacho ni kiima siyo lazima kidhihirishe sifa hizi zote kwa wakati mmoja. Mfano Na. 11 unaonesha kiambajengo ambacho ni kiima katika tungo.

11. *M-toto a-me-lal-a sakafu-ni*
Kng1-toto kk1- tmlf- lal- kt kng9.sakafu –ktm
Mtoto amelala sakafuni.'

Mfano Na. 11 unaonesha kwamba kiambajengo *mtoto* ni kiima kwa sababu kinatokea mwanzoni mwa sentensi kabla ya kitenzi, kinaukilia upatanishi wa kisarufi na kitenzi *amelala* kwa kutumia kiambishi cha upatanishi wa ngeli ya 1 (kk1) ambacho ni {*a*-}.

**(b) Yambwa**

Yambwa ni dhima ya kisarufi inayofanywa na kiambajengo cha sentensi. Kiambajengo hicho kinadhihirisha sifa kadhaa. Sifa ya kwanza ni kwamba, kisintaksia, yambwa hutokea mara baada ya kitenzi katika sentensi. Kuhusiana na nafasi ya yambwa, Hyman na Duranti (1982) wanaeleza kuwa yambwa hutokea mara baada ya kitenzi katika sentensi yenye mfuatano wa kawaida wa viambajengo vyake. Sifa ya pili ni kwamba, kifonolojia, yambwa ina mfungamano wa kimatamshi na kitenzi. Kwa kawaida, kuna mfungamano wa kimatamshi baina ya kipashio ambacho kinatokea mara baada ya kitenzi na kitenzi chenyewe. Mfungamano huo unazingatia kanuni ya urefushaji wa irabu ya mwisho kaso moja katika kirai kitenzi. Sifa ya tatu ni kwamba yambwa inaweza kuwa na dhima tofauti za kisemantiki na dhima hizo ni kama muathirika, kithimu na mnufaika. Sifa ya nne ni kwamba neno au kirai ambacho ni yambwa huweza kuwakilishwa na kiambishi yambwa katika kitenzi. Hata hivyo, uwekaji wa kiambishi yambwa hutegemea muundo wa lugha inayohusika. Lugha hutofautiana katika idadi na taratibu za uwekaji wa kiambishi cha yambwa katika kitenzi. Kuna lugha zinaruhusu uwekaji wa kiambishi yambwa kimoja, na nyingine zinaruhusu kiambishi yambwa zaidi ya kimoja. Mathalani, Kiswahili ni mfano wa lugha zinazoruhusu uwekaji wa kiambishi yambwa kimoja. Pia, nafasi ya kiambishi yambwa katika kitenzi, hutofautiana kati ya lugha moja na nyingine. Kuna lugha kama vile Kiyao (P21, Tanzania) huweka kiambishi yambwa kabla ya mzizi wa kitenzi; lugha nyingine kama vile Kikonzime (A84, Cameroon) huweka baada ya kiambishi tamati cha kitenzi; na lugha nyingine kama vile Kilunda (L52, Zambia) huweka kabla ya mzizi na baada ya kiambishi tamati. Kiswahili ni mfano wa lugha ambazo huweka kiambishi yambwa kabla ya mzizi wa kitenzi. Aidha, katika lugha za Kibantu, uwekaji wa kiambishi cha yambwa hutegemea vigezo viwili. Kigezo cha kwanza ni uhisivu wa yambwa inayorejelewa (Wald, 1979; Hyman na Duranti, 1982; Keach, 1995). Kwa kawaida, kiambishi yambwa huambikwa katika kitenzi iwapo yambwa inayorejelewa ni nomino hisivu kutoka katika ngeli ya kwanza au ya pili. Iwapo yambwa ni nomino za ngeli nyingine, basi kiambishi yambwa siyo cha lazima katika kitenzi. Kigezo cha pili ni umahususi wa yambwa inayorejelewa (Givon, 1976; Allan, 1983)[5]. Katika kigezo hiki, kiambishi yambwa huwekwa iwapo yambwa inayorejelewa ni mahususi. Kwa hiyo, kutokana na sifa zilizotolewa, yambwa ni istilahi ya kiuamilifu. Mfano Na. 12 unaonesha istilahi ya kiambajengo ambacho ni yambwa:

---

[5] Dhana ya umahususi pia inaweza kueleweka kwa maana ya mkazo, utofauti na upekee.

12. *M-toto a-na-m-pig- a* <u>*mbuzi*</u>
Kng1-toto kk1- knj- ky1- pig- kt <u>kng1.mbuzi</u>
'Mtoto anampiga mbuzi.'

Mfano Na. 12 unaonesha kiambajengo ambacho kina uamilifu wa yambwa katika tungo. Katika mfano huu, kiambajengo *mbuzi* ni yambwa kwa sababu kinatokea baada ya kitenzi katika nafasi ya yambwa mara baada ya kitenzi *anampiga*. Pia, neno mbuzi limerejelewa na kiambishi yambwa {-m-}. Hivyo, yambwa ni istilahi ya uamilifu wa kiambajengo katika tungo.

**(c) Yambwa$_{\theta}$**

Ni dhima ya kisarufi inayofanywa na kiambajengo cha sentensi chenye sifa kadhaa. Mosi, kama ilivyo kwa yambwa, neno au kirai kinachofanya kazi kama yambwa$_{\theta}$, kisintaksia hutokea mara baada ya kitenzi. Pili, huonesha mfungamano wa kimatamshi na kitenzi katika sentensi. Hata hivyo, yambwa$_{\theta}$ na yambwa hutofautiana kama ifuatavyo: mosi, hakiwezi kupinduliwa na kuwa kiima cha sentensi tendwa. Pili, huhusishwa na dhima ya kisemantiki mahususi; na mara nyingi, huhusishwa na dhima ya kisemantiki ya kithimu au muathirika. Tatu, hakiwezi kuwakilishwa na kiambishi yambwa katika kitenzi. Zaidi ya hayo, hakiwezi kufanyiwa urejeshaji kama ilivyo kwa kipashio chenye dhima ya yambwa. Kutokana na sifa hizi, yambwa$_{\theta}$ ni istilahi ya kiuamilifu. Mfano Na. 13 unaonesha kiambajengo ambcho kina uamilifu wa yambwa$_{\theta}$:

(13) *Ki-jiji-ni ku-me-ene-a*<u>*u-gonjwa*</u>
Kng7-jiji-ktm kk17- ktmlf- ene- kt <u>kng14-gonjwa</u>
'Kijijini kumeenea ugonjwa.'

Mfano Na. 13 unaonesha kuwa kiambajengo *ugonjwa* ni yambwa$_{\theta}$ kwa sababu kinatokea baada ya kitenzi katika nafasi ya yambwa. Licha ya kutokea katika nafasi hiyo, kiambajengo hiki hakiwezi kurejelewa na kiambaishi yambwa katika kitenzi. Ikifanyika hivyo, inazalishwa tungo isiyokubalika katika Kiswahili. Mathalani, **Kijijini kumeuenea ugonjwa* ni tungo ambayo haikubaliki kisintaksia katika Kiswahili. Kwa hiyo, yambwa$_{\theta}$ ni istilahi inayotumika kuonesha uamilifu wa kiambajengo katika tungo.

**(d) Yambiwa**

Yambiwa ni istilahi ya kiuamilifu inayofanywa na kiambajengo katika sentensi. Kiambajengo kinachofanya kazi ya yambiwa huhesabika kama yambwa ya pili katika sentensi. Hata hivyo, kiambajengo hicho sio yambwa kwa sababu licha ya kutokea baada ya kitenzi hakina uhusiano wa moja kwa moja na kitenzi. Aidha, kiambajengo hiki hakiwakilishwi na kiambishi yambwa katika kitenzi. Pia, kuwapo kwake kunategemea kuwapo kwa yambwa katika sentensi. Mfano Na. (14) unaonesha yambiwa katika lugha ya Kiswahili:

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **(**14**)** | *Mama* | *a-* | *na-* | *m-* | *pik-* | *i-* | *a* | *m-toto* | <u>*ch-akula*</u> |
| | kng1.mama | kk1- | knj- | kny1- | pik- | ktnda- | kt | kng1-toto | <u>kng7-akula</u> |

‘Mama anampikia mtoto chakula.’

Mfano Na. (14) unaonesha kwamba kiambajengo *chakula* kina uamilifu wa yambiwa katika tungo. Kiambajengo hiki kinatokea baada ya kitenzi *anampikia* mara baada ya yambwa *mtoto*. Kiambajengo hiki hakijawakilishwa na yambwa katika tungo. Hakijawakilishwa na kiambishi yambwa kwa sababu hakina uhusiano wa moja kwa moja na kitenzi kinachohusika.

**(e) Oblikyu$_{\theta}$**

Hii ni dhima ya kisarufi inayofanywa na neno au kirai katika sentensi. Kama yambwa$_{\theta}$, pia oblikyu$_{\emptyset}$ inahusishwa na dhima moja mahususi ya kisemantiki. Dhima hiyo inaweza kuwa ni ya umahali au ala. Aidha, tofauti na yambwa$_{\theta}$, neno au kirai chenye dhima ya oblikyu$_{\emptyset,}$ kifonolojia hakioneshi mfungamano wa kimatamshi na kitenzi. Katika lugha za Kibantu, kimahali au kiala ambacho hutokea baada ya kitenzi kinahusishwa na dhima ya oblikyu$_{\theta}$. Mfano Na. 15 unaonesha kiambajengo ambacho kina uamilifu wa oblikyu$_{\theta}$:

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (15) | *Maji* | *ya-* | *me-* | *ja-* | *a* | <u>*bahari-ni*</u> |
| | kng6.maji | kk6- | tmlf- | ja- | kt | <u>kng9.bahari -ktm</u> |

‘Maji yamejaa baharini.’

Mfano Na. 15 unaonesha kwamba kiambajengo *baharini* ni oblikyu$_{\theta}$ kwa sababu kinatokea baada ya kitenzi katika nafasi ya yambwa. Pia, kiambajengo hiki kinahusishwa na dhima mahususi ya kisemantiki. Dhima hiyo ni ya umahali. Kwa hiyo, oblikyu$_{\theta}$ ni istilahi ya uamilifu wa kiambajengo.

**(f) Kijalizo**

Kijalizo ni istilahi inayorejelea uamilifu wa kiambajengo katika sentensi. Dowty (2000) anaeleza sifa za msingi za kijalizo ambazo zinatumiwa na wanaisimu katika kukibainisha. Kisemantiki, anaeleza kijalizo kuwa ni kipashio ambacho kinakamilisha maana katika tungo. Kisintaksia, kijalizo ni kipashio cha lazima ambacho hakiwezi kuondolewa katika tungo bila kuleta athari ya kisarufi. Kwa ujumla, kijalizo ni dhima ya kisarufi inayofanywa na neno au kirai msingi ambacho kinakamilisha maana katika tungo. Aidha, neno au kirai hicho hakiwezi kuondolewa bila kuleta athari za kisarufi katika tungo inayohusika. Mfano Na. 16 unaonesha kiambajengo ambacho kina dhima ya ujalizaji katika tungo:

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (16) | *Nyoka* | *a-* | *me-* | *ingi-* | *a* | <u>*pango-ni*</u> |
| | kng1.nyoka | kk1- | tmlf- | ingi- | kt | <u>kng5.pango-ktm</u> |

‘Nyoka ameingia pangoni.’

Mfano Na. 16 unaonesha kuwa kiambajengo *pangoni* ni kijalizo kwa sababu

kinakamilisha maana ya sentensi. Kiambajengo hiki kikiondolewa, inazalishwa tungo isiyokubalika katika Kiswahili. Kwa hiyo, kijalizo ni istilahi ya uamilifu wa kiambajengo.

**(g) Chagizo**

Chagizo, ni istilahi inayorejelea uamilifu wa kiambajengo katika sentensi. Kwa mujibu wa TUKI (1990), chagizo ni kipashio ambacho kinatumika kama nyongeza ya maana, na ambacho kinaweza kuondolewa bila kuathiri maana ya msingi ya sentensi. Kwa ujumla, tunaweza kusema kwamba chagizo ni kipashio cha hiari ambacho kinatumika kufafanua au kuongeza maana katika tungo. Kipashio hiki kinaweza kuondolewa bila kuleta athari ya kisarufi katika tungo inayohusika. Vilevile, kipashio hiki siyo sehemu ya semantiki ya kitenzi na wala hakichangii katika kukamilisha semantiki ya kitenzi. Mfano Na. 17 unaonesha chagizo katika Kiswahili:

(17) *M-toto a-na-li-\ <u>sana</u>*
Kng1-toto kk1- knj- li- kt <u>sana</u>
'Mtoto analia sana.'

Mfano wa 17 unaonesha kuwa *sana* ni chagizo. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba chagizo ni istilahi inayotumika kuonesha uamilifu wa kiambajengo katika tungo.

**(h) Neno Kuu au Kiini**

Ni sehemu ya kirai ambayo ni kiini au mhimili wa kirai. Kutokana na kanuni ya Uneno kuu, kila kirai lazima kiwe na neno kuu. Neno kuu ndilo linalopatia jina kirai husika. Kwa kawaida kuna aina kuu mbili za neno kuu zinazojibainisha katika lugha mbalimbali. Uainishaji wa aina hizi umetokana na sifa ya ujitoshelezi wa neno kuu husika. Kwanza, kuna neno kuu ndani (*endocentric headword*). Hili ni neno kuu linaloweza kusimama peke yake bila ya kuwepo kwa kijalizo. Mathalani, neno kuu katika KN, KV, KT na KE. Pili, ni neno kuu nje (*exocentric headword*). Hili ni neno kuu ambalo haliwezi kusimama peke yake bila kutegemea kuwepo kwa kijalizo. Likisimama peke yake halijitoshelezi kimuundo na kimaana. Neno kuu hili linapatikana katika KH. Mfano Na. 17 (a) unaonesha neno kuu ndani na mfano Na. 18 (b) unaonesha neno kuu nje:

(18) a) *<u>m-toto</u> m-dogo a-na-li-a*
*<u>kng1-toto</u> kv1-dogo kk1-knj-li-kt*
'Mtoto mdogo analia'
b) *m-zee <u>w-a</u> busara a-me-ondo-a*
*kng1-zee <u>kh1-a</u>` kng9 kk1-kjn-ondo-kt*
'Mzee wa busara ameondoka'

Mfano Na. 17 (a) unaonesha kwamba katika kirai nomino (KN) *mtoto mdogo*, *mtoto* ni neno kuu. Aidha, mfano Na. 18 (b) unaonesha kwamba katika kirai kihusishi (KH) *wa busara*, *wa* ni neno kuu nje. Kwa ujumla, neno kuu au kiini ni istilahi ya kiuamilifu.

Kwa ujumla, istilahi zilizofafanuliwa katika sehemu hii zinaonesha uamilifu wa viambajengo vya sentensi. Zinapotumika zinarejelea uchanganuzi kwa kutumia Mkabala wa Uamilifu wa Viambajengo. Ufafanuzi huu unaonesha ni kwa namna gani unaweza kuchanganua viambajengo kiuamilifu kwa kutumia istilahi za kiuamilifu. Kwa kuzingatia data zilizokusanywa kutoka katika changanuzi mbalimbali za watoataarifa, mkabala huu unaondoa changamoto ya kuchanganya istilahi za kiuamilifu na kimuundo (taz. Philipo, 2018). Mkabala huu ni faafu kwa sababu unaonesha kwamba kiambajengo kinachohusika kina uamifu gani wa kisarufi katika tungo. Hata hivyo, pamoja na ufaafu wake, mkabala huu hauoneshi ni kwa namna gani kiambajengo hicho kinaungana na kiambajengo kingine ili kuunda kiambajengo kikubwa zaidi. Pia, hauoneshi kiambajengo hicho kinawakilisha dhima ipi ya kisemantiki au taarifa gani katika tungo. Kwa hiyo, uchanganuzi wa viambajengo unaweza kufanywa pia kwa kutumia Mkabala wa Vishiriki vya Kitenzi kama inavyofafanuliwa katika sehemu 4.3.

### 4.3 Mkabala wa Vishiriki vya Kitenzi

Huu ni mkabala unaozingatia dhima za kisemantiki za vishiriki vya kitenzi kinachounda sentensi. Mkabala huu unaonesha kuwa kitenzi kinaweza kuambatana na vishiriki vingapi na, vishiriki hivyo vina dhima zipi za kisemantiki. Dhima za kisemantiki ni uamilifu wa kisemantiki unaofanywa na virai nomino na virai vihusishi ambavyo ni vishiriki vya kitenzi kinachounda tungo. Kielelezo Na. 3 kinaonesha Mkabala wa Vishiriki vya Kitenzi wa kitenzi *kula* ambacho kinaunda sentensi *Mtoto anakula*.

**Kielelezo Na. 3: Vishiriki vya Kitenzi**

*Mtoto anakula chakula*.

*anakula* <Mtenda, kiathirika>

Mtoto Chakula

Kielelezo Na. 3 kinaonesha kuwa kitenzi *anakula* kinahitaji vishiriki viwili ambavyo ni mtenda na kiathirika. Mtenda ni *mtoto* na kiathirika ni *chakula*.

#### 4.3.1 Istilahi za Kisemantiki

Hizi ni istilahi zinazohusu uamilifu wa kisemantiki wa vishiriki vya kitenzi kinachounda sentensi. Muundo wa kitenzi una idadi na dhima za kisemantiki za vishiriki vinavyoweza kuambatana na kitenzi hicho (taz. Fillmore, 1968). Bresnan na Kanerva (1989). Wataalamu hawa wanataja dhima hizo kuwa ni mtenda, mnufaika, mpokeaji, mweksiperiensa, kithimu, kiathirika, ala na kimahali. Idadi hii ni sawa na ya Givon (2001) ambaye anatambua dhima nane za kisemantiki. Dhima hizo ni mtenda, kiathirika, kidativu, ala, mnufaika, kimahali, kihusianishi na kinamna. Pia, Kroeger (2004) anaorodhesha dhima kumi za kisemantiki ambazo ni mtenda, mweksiperiensa, mpokeaji, mnufaika, ala, kithimu, kiathirika, mstuliwa, kimahali na kihusianishi. Mkude (2005) anataja dhima za kisemantiki ambazo

zinajitokeza katika Kiswahili kuwa ni mtenda, mnufaika, kithimu, kiathirika, kimahali na kiala. Licha ya kuwapo kwa dhima nyingi ambazo zimefafanuliwa na baadhi ya wanaisimu ambao tumewataja hapo juu, katika makala haya tumejadili dhima sita kwa sababu ndizo zinazojitokeza katika data tulizozikusanya. Dhima hizo ni mtenda, kimahali, kithimu, kiathirika, mnufaika na kiala.

**(a) Mtenda**

Mtenda ni dhima ya kisemantiki ambayo inawakilisha mtendaji wa tendo. Kwa kawaida, mtenda katika lugha za Kibantu ana sifa za uhisivu kama ilivyo katika mfano wa 18 (a). Kwa mantiki hiyo, anaweza kuwa binadamu, mnyama, au mdudu. Hata hivyo, mtenda anaweza kuwa kitu kisicho na uhisivu kama ilivyo katika mfano wa 18 (b):

(18) a) *Juma anasoma kitabu.*
b) *Mvua imeharibu mazao.*

Mfano wa 18 (a) unaonesha kuwa *Juma* ni mtenda ambaye kimsingi ana sifa ya uhisivu. Mfano wa 18 (b) unaonesha kuwa *mvua* ni mtenda ambaye kimsingi hana sifa ya uhisivu. Kwa hiyo, mtenda katika Kiswahili anaweza kuwa hisivu au sihisivu.

**(b) Kimahali**

Kimahali ni istilahi inayorejelea kiambajengo kinachowakilisha mahali pa jumla, mahususi au ndani. Katika lugha nyingi za Kibantu, kama vile Kichewa (N31, Malawi), maneno yanayorejelea mahali huambikwa viambishi vya ngeli za mahali 16 **pa*-, 17 **ku*-, au 18 **mu*-[6] mwanzoni mwa mashina yake. Katika lugha nyingine, kama vile Kikuyu (E51, Kenya), maneno hayo yanaambikwa kiambishi tamati cha mahali -*ni/ng*. Katika Kiswahili, maneno hayo huambikwa kiambishi tamati cha mahali -*ni* mwishoni mwa mizizi yake (taz. Polome, 1967; Mkude, 2005; Amidu, 2007). Katika lugha ya Kiswahili kiambishi *ni* huambikwa mwishoni mwa nomino na hivyo huwa kama kiambishi tamati cha mahali. Kiambishi tamati katika nomino za Kiswahili kinafanya kazi badala ya viambishi vya ngeli za mahali (Polome, 1967). Kiambishi hiki, kama ilivyo katika lugha nyingine za Kibantu kama vile Kikuyu (E51, Kenya), kinatumika kunyambua nomino za ngeli nyingine na kuzifanya kuwa nomino za mahali. Mifano ya 19 (a) na 19 (b) inaonesha vimahali katika Kiswahili:

(19) a) Nyoka ameingia shimoni.
b) Mwalimu anaandika ubaoni.

Mifano Na. 19 (a) na 19 (b) inaonesha viambajengo ambavyo ni vimahali katika Kiswahili. Viambajengo hivyo vimeambikwa kiambishi tamati cha umahali {-*ni*}.

[6] Kiambishi *pa*- hurejelea mahali karibu, mahususi, panapojulikana au juu. Aidha, kiambishi *ku*- hurejelea mahali ambapo ni mbali, pa jumla ambapo siyo lazima pajulikane, au uelekeo. Aidha, kiambishi *mu*- hurejelea mahali ndani.

Hata hivyo, vipo vimahali ambavyo havijaambikwa kiambishi hiki lakini vinataja majina ya mahali kama inavyoonekana katika mfano Na. 20 (a). Pia, vipo vimahali ambavyo vimeundwa na vihusihi vya mahali na vinarejelea vimahali katika lugha ya Kiswahili kama inavyoonekana katika mfano Na. 20 (b):

(20) a) Baba ameenda Dodoma.
b) Kitabu kipo juu ya meza.

Mfano Na. 20 (a) unaonesha kwamba kiambajengo *Dodoma* ni kimahali. Pia, katika mfano Na. 20 (b), kiambajengo *juu ya meza* ni kimahali. Kwa hiyo, kimahali ni istilahi inayohusu dhima ya kisemantiki.

**(c) Kithimu**

Kithimu ni istilahi inayorejelea mtu, mnyama, kiumbe, au kitu kinachohusishwa na mahali. Aidha, mtu, mnyama, kiumbe, au kitu hicho huweza kuonesha mabadiliko ya mahali kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Mifano ya 21 (a) na 21 (b) inaonesha vithimu katika lugha ya Kiswahili:

(21) a) Taka zimeenea kiwanjani.
b) Mdudu ameingia shimoni.

Katika mifano ya 21 (a) na 21 (b), *taka* na *mdudu* ni vithimu. Kithimu *taka* kinahusishwa na mahali kulikoenea taka, yaani *kiwanjani*. Aidha, kithimu *mdudu* kinaonesha kubadilisha mahali ambapo mwanzoni alikuwa sehemu fulani na sasa yumo *shimoni*. Kwa hiyo, kithimu pia ni istilahi inayorejelea dhima ya kisemantiki ya kiambajengo.

**(d) Kiathirika**

Kiathirika ni mtu au kitu ambacho kimepata athari ya tendo moja kwa moja. Athari hiyo inaweza kuwa ya mabadiliko ya kiumbo, kirangi, kimuonekano na kadhalika. Mifano Na. 22 (a) na 22 (b) inaonesha viathirika katika Kiswahili:

(22) a) Mama amempiga mtoto.
b) Mtoto anakula chakula.

Katika mifano Na. 22 (a) na 22 (b), *mtoto* na *chakula* ni viathirika kwa sababu ndivyo vilivyopata athari za tendo la kupiga na lile la kula mtawalia.

**(e) Mnufaika**

Mnufaika ni mtu, kiumbe au kitu ambacho manufaa ya tendo yameelekezwa kwake. Mifano Na. 23 (a) na 23 (b) inaonesha mnufaika katika sentensi za Kiswahili:

(23) a) Mama anamlisha mtoto chakula.
b) Mama anampikia baba chakula.

Katika mifano Na. 23 (a) na 23 (b), *mtoto* na *baba* ni wanufaika kwa sababu manufaa ya tendo la kulisha na kupika yanaelekezwa kwao. Kwa hiyo, istilahi mnufaika hurejelea dhima ya kisemantiki katika Kiswahili.

**(f) Kiala**

Kiala ni istilahi inayorejelea kifaa kilichotumika kutendea tendo linalotajwa katika sentensi. Mifano Na. 24 (a) na 24 (b) inaonesha viala katika sentensi za Kiswahili.


(24) a) Juma amekatia kisu.
b) Mama amepikia sufuria.

Katika mifano Na. 24 (a) na 24 (b), *kisu* na *sufuria* ni viala kwa sababu ndivyo vilivyotumika katika tendo la kukata na kupika, mtawalia. Kwa hiyo, istilahi kiala hurejelea dhima ya kisemantiki katika Kiswahili. Kwa ujumla, istilahi hizi zinarejelea dhima za kisemantiki za viambajengo mbalimbali vya sentensi. Pia, zinaambatana na uchanganuzi wa viambajengo vya sentensi kwa kutumia Mkabala wa Vishiriki vya Kitenzi. Mkabala huu ni faafu kwa sababu unadokeza dhima za kisemantiki zinazowakilishwa na viambajengo vya sentensi. Hata hivyo, mkabala huu hauoneshi uambajengo wa sentensi, uamilifu wa kisarufi wa viamabajengo hivyo na muundo wa taarifa unaowakilishwa na viambajengo hivyo. Kwa hiyo, uchanganuzi wa viambajengo unaweza kufanywa kwa kutumia mikabala mingine kama ilivyofafanuliwa na sehemu zilizotangulia. Pia, unaweza kufanywa kwa kutumia Mkabala wa Muundo wa Taarifa kama inavyofafanuliwa katika sehemu 4.4.

**4.4 Mkabala wa Muundo Taarifa**

Huu ni mkabala wa uchanganuzi wa viambajengo vya sentensi kwa kuzingatia muundo wa taarifa wa sentensi kipragmatiki (kimawasiliano). Bresnan na Mchombo (1987) wanafafanua muundo wa taarifa katika tungo, yaani aina ya taarifa na sifa za kimofosintaksia zinazoambatana na viambajengo vinavyowasilisha taarifa hizo. Kwa mujibu wao, sentensi ina taarifa ambayo ni mada na ile ambayo ni fokasi. Taarifa hizi zinawakilishwa na viambajengo vya sentensi vinavyoweza kuchanganuliwa kwa kutumia Mkabala wa Muundo wa Taarifa kama inavyoonekana hapa chini:

**Kielelezo Na. 4: Muundo wa Taarifa**




Kielelezo Na. 4 kinaonesha muundo wa taarifa wa sentensi *Mtoto anakula chakula*. Kinaonesha kwamba mada inawasilishwa na kiambajengo ambacho ni *mtoto*. Fokasi inawaweza kuwakilishwa na kiambajengo *anakula chakula*, *anakula* au *chakula*.

### 4.4.1 Istilahi Zinazorejelea Muundo wa Taarifa

Uchanganuzi wa viambajengo vya sentensi kwa kutumia Mkabala wa Muundo wa Taarifa huambatana na matumizi ya istilahi mbili ambazo ni mada na fokasi.

**(a) Mada**

*Mada* ni taarifa ambayo inajulikana katika tungo. Katika Kielelezo Na. 4, kiambajengo *mtoto* ni mada kwa kuwa kina sifa kadhaa za mada katika tungo hii. Mosi, kiambajengo hiki ni kiima cha sentensi. Bresnan na Mchombo (1987) na Ndung'u (2015) wanaeleza kwamba mada ni taarifa ambayo huwakilishwa na kiambajengo cha kwanza (ambacho kiuamilifu ni kiima) katika mpangilio wa kawaida wa viambajengo. Katika Kielelezo Na. 4, tunaona kwamba kiambajengo *mtoto* ni kiima katika tungo *Mtoto anakula chakula*. Hivyo, kiambajengo *mtoto* ni mada katika tungo hii.

Pili, kiambajengo *mtoto* ni mada kwa sababu kinaweza kurejeshwa. Kwa mujibu wa Bresnan na Mchombo (1987), mada ni taarifa ambayo inaweza kuwakilishwa na kiambajengo kinachoweza kurejeshwa na kuwakilishwa na kiambishi rejeshi katika kitenzi. Kutokana na data zilizokusanywa, kiambajengo *mtoto* katika tungo hii kinaweza kurejeshwa na kuwakilishwa na kiambishi rejeshi katika kitenzi kinachounda kishazi rejeshi. Mfano Na. 25 unathibitisha hoja hii:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| (25) ***M-toto*** | *a-li-**ye**-pita- a* | | *a-na-ku-l-a* | *ch-akula* |
| kng1- | toto | kk1-knj-krj1-pit-kt | kk1-knj-ksuk-l-kt | kng7-akula |

'Mtoto aliyepita anakula chakula.'

Mfano Na. 25 unaonesha kishazi rejeshi *mtoto aliyepita*. Kiambajengo *mtoto* ni mada kwa kuwa kimerejeshwa na kuwakilishwa na kiambishi rejeshi -*ye*-.

**(b) Fokasi**

Fokasi ni taarifa mpya na inayosisitizwa katika tungo. Aidha, fokasi inaweza kuwa nyembamba ama pana. Fokasi nyembemba huhusu kiambajengo kimoja mahususi katika sentensi. Hii ni taarifa inayowakilishwa na neno moja katika sentensi. Fokasi pana inahusu kiambajengo kipana katika sentensi. Hivyo, hii ni taarifa inayowakilishwa na maneno mawili au zaidi katika kiwango cha kirai. Kiambajengo kinachowakilisha fokasi huweza kuulizwa katika tungo. Inaweza kuulizwa kwa kuwa kiulizi kinahusishwa na taarifa mpya ambayo haijulikani kwa mpokeaji wa taarifa hiyo. Kwa hiyo, katika mfano Na. 26, kiambajengo *chakula* katika tungo ni fokasi nyembamba kwa kuwa kiambajeno hiki kinaweza kuulizwa kwa kutumia neno ulizi *nini* katika nafasi yake. Mifano Na. 26 (a) na 26 (b) inathibitisha hoja hii:

(26) a) Mtoto anakula <u>chakula</u>
b) Mtoto anakula <u>nini</u>?

Mfano Na. 26 (a) unaonesha kwamba kiambajengo *chakula* ni fokasi kwa sababu katika mfano Na. 26 (b) kimeweza kuulizwa kwa kutumia neno ulizi *nini*?

Pili, kiambajengo *chakula* katika tungo hii ni fokasi kwa kuwa hakiwezi kurejelewa ama kuwakilishwa na kiambishi yambwa katika kitenzi. Kwa kuzingatia data zilizokusanywa, kiambajengo hiki kikirejelewa na kiambishi yambwa huzalisha tungo isiyokubalika katika lugha ya Kiswahili. Mifano Na. 27 (a) na 27 (b) inathibitisha hoja hii:

(27) a) **M-toto* *a-na-**ki**-ku-l-a* ***ch-akula***
kng1-toto kk1-knj-**ky7**-ksuk-l-kt **kng7**-akula
'*Mtoto anakikula chakula.'

b) **M-toto* *a-na-**ki**-ku-l-a*
kng1-toto kk1-knj-**ky7**-ksuk-l-kt
'*Mtoto anakikula.'

Mfano wa 27 (a) unaonesha kuwa kiambajengo *chakula* hakiwezi kurejelewa na ky *-ki-* katika kitenzi *anakula* (kitenzi ni *anakula* sio **anala*). Kuwapo kwa ky {–ki-} kunazalisha tungo isiyokubalika. Mfano wa 29 (b) unaonesha kuwa kiambajengo *chakula* hakiwezi kuwakilishwa na ky {-*ki*-}. Kuwapo kwa kiambishi hiki kunazalisha tungo isiyokubalika. Hivyo, kiambajengo *chakula* ni fokasi nyembamba kwa kuwa kina tabia ya fokasi ya kutoweza kuwakilishwa na ky.

Istilahi mada na fokasi zinatumika tunapochanganua viambajengo kwa kutumia Mkabala wa Muundo Taarifa. Mkabala huu ni mzuri kwa sababu unaonesha aina ya taarifa inayowakilishwa na viambajengo vya sentensi. Pia, unaondoa changamoto ya kuchanganya istilahi za kimawasiliano na zile za miundo mingine kama ilivyokuwa inafanywa hapo awali. Hata hivyo, mkabala huu haujitoshelezi kwa sababu hauoneshi uambajengo wa sentensi wala uamilifu wa viamabajengo vya sentensi. Hivyo, ili kudokeza taarifa hizo, uchanganuzi wa viambajengo vya sentensi unaweza kufanywa kwa kutumia mikabala mingine kama ilivyofafanuliwa katika sehemu 4.1, 4.2 na 4.3.

**5.0 Hitimisho**

Kwa ujumla, makala haya yamebainisha na kufafanua mikabala ya uchanganuzi wa viambajengo vya sentensi na istilahi zinazotumika kwa kutumia mifano ya lugha ya Kiswahili. Katika ufafanuzi huo, kwa kutumia misingi ya Nadharia ya Sarufi Leksia Amilifu ya Bresnan na Kaplan (mwishoni mwa miaka ya 1970), imefafanua mikabala minne ambayo ni Mkabala wa Miundo ya Viambajengo, Mkabala wa Uamilifu wa Viambajengo, Mkabala wa Vishiriki vya Kitenzi na Mkabala wa Muundo wa Taarifa. Baada ya ufafanuzi huo, makala pia yamefafanua istilahi zinazotumika kwa kila mkabala. Istilahi zinazotumika katika Mkabala wa Miundo ya Viambajengo ni kama vile sentensi sahihi, sentensi changamani, sentensi ambatani, kishazi, kishazi huru, kishazi tegemezi, kirai nomino, kirai kitenzi, kirai kivumishi, kirai kielezi na kirai kihusishi. Istilahi nyingine ni nomino, kitenzi, kivumishi, kielezi na kihusishi. Kuhusu Mkabala wa Uamilifu wa Viambajengo, makala yamefafanua kwamba viambajengo vya sentensi huchanganuliwa kwa kuzingatia uamilifu wake. Aidha, istilahi zinazotumika katika

mkabala huu ni kama vile kiima, yambwa, yambiwa, chagizo na kijalizo. Vilevile, kuhusu Mkabala wa Vishiriki vya Kitenzi, makala yameeleza kwamba viambajengo vya sentensi huchanganuliwa kwa kuzingatia dhima za kisemantiki za vishiriki vya kitenzi kinachounda sentensi. Kwa kuzingatia msingi huo, istilahi zinazotumika ni zile zinazorejelea dhima za kisemantiki. Mifano ya istilahi hizo ni mtenda, kimahali, kithimu, kiathirika, mnufaika na kiala. Pia, katika Mkabala wa Muundo wa Taarifa, makala yameeleza kwamba uchanganuzi wa viambajengo vya sentensi unafanywa kwa kuzingatia muundo wa taarifa unaowakilishwa na viambajengo vya sentensi. Kwa kuzingatia msingi huo, istilahi zinazotumika katika mkabala huu ni mada na fokasi. Kwa hiyo, makala yameweka wazi kwamba sentensi moja inaweza kuchanganuliwa kwa kutumia mikabala minne tofauti. Licha ya kuweza kufanya hivyo, kila mkabala unatumia istilahi zake zinazotambulisha mkabala unaohusika. Istilahi za mkabala mmoja hazipaswi kuchanganywa katika mkabala mwingine.

**Alama na Vifupisho vilivyotumika**

| | | |
|---|---|---|
| kh | = | kipatanishi cha kihusishi |
| kir | = | kirejeshi |
| kk | = | kipatanishi cha kiima |
| knj | = | kiambishi njeo |
| ksuk | = | kiambishi siukomo |
| kt | = | kiambishi tamati |
| ktm | = | kiambishi tamati mahali |
| ktndk | = | kiambishi cha utendeka |
| kv | = | kipatanishi cha kivumishi |
| ktndn | = | kiambishi cha utendana |
| ky | = | kiambishi yambwa |
| MMT | = | Mkabala wa Muundo Taarifa |
| MMV | = | Mkabala wa Miundo ya Viambajengo |
| MUV | = | Mkabala wa Uamilifu wa Viambajengo |
| MVK | = | Mkabala wa Vishiriki vya Kitenzi |
| PRED | = | Prediketa |
| SLA | = | Sarufi Leksia Amilifu |
| tmlf | = | timilifu |

**Marejeleo**


Allan, K. (1983). Anaphora, Cataphora, and Topic Focusing: Function of Object Prefix in Swahili. Katika I. Dihoff (Mh.), *Current Approaches to African Linguistics* (uk. 323 – 335). Foris: Doridrecht.

Allan, K. (1983). Anaphora, Cataphora, and Topic Focusing: Function of Object Prefix in Swahili. Katika I. Dihoff (Mh.), *Current Approaches to African Linguistics* (Kur.. 323 – 335). Foris: Doridrecht.

Besha, R. (1994). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Bresnan, J. na Kanerva, J. M. (1989). “Locative Inversion in Chichewa: A Case

Study of Factorization in Grammar". *Linguistic Inquiry*, 20: 1- 50.
Bresnan, J. na Mchombo, S. A. (1987). "Topic, Pronoun, and Agreemant in Chichewa". *Language*, 63: 741 - 782.
Dowty, D. (2000). "The Dual Analysis of Adjuncts/Complements in Categorial Grammar". *ZAS Papers in Linguitics*, 17: 1 - 26.
Fillmore, C. (1968). The Case for Case. Katika E. Bach na R. T. Harms (Wah.), *Universals in Linguistic Theory* (uk. 1 – 90). New York: Holt, Rinehart and Winston.
Givon, T. (1976). Topic, Pronoun, and Grammatical Agreement. Katika C. Li (Mh.), *Subject and Topic* (uk. 149 – 188). New York: Academic Press.
Givon, T. (2001). *Syntax: An Introduction*. Amsterdam/Philadelphia: John Benjamins.
Hyman, L. M. na Duranti, A. (1982). "On the Object Relation in Bantu". *Syntax and Semantics*, 15: 217 - 239.
Keach, C. N. (1995). Subject and Object Markers as Agreement and Pronominal Incorporation in Swahili. Katika A. Akinbiyi (Mh.), *Theoretical Approaches to African Linguistics*. New York: Trenton. Kur. 109 – 116.
Keenan, E. L. (1976). Towards a Universal Definition of Subject. Katika C. N. Li, (Mh.), *Subject and Topic* (Kur. 303 – 333). New York: Academic Press.
Kroeger, P. R. (2004). *Analysing Syntax: A lexical Functional Approach*. Cambridge: Cambridge University Press.
Mkude, D. J. (2005). *The Passive Constructions in Swahili*. Tokyo: Research Institute for Languages and Cultures of Asia and Africa (ILCAA).
Massamba, D. P. B, Kihore, Y. M. na Hokororo, J. I. (2000). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.
Ngung'u, N. M. (2015.). "Information Structure in Kiswahili". *International Journal of Education and Research*, 3(3): 309 – 320.
Phillipo, Z. T. (2018). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Dar es Salaam: Karljamer Publishers Limited.
Philipo, Z. T. na Kuyenga, F. E. (2018). *Sintaksia ya Kiswahili: Nadharia za Kisintaksia na Uchanganuzi wa Kiswahili*. Dar es Salaam: Karljamar Publishers LTD.
Polomé, E. C. (1967). *Swahili Language Handbook*. Washington DC: Center for Applied Linguistics.
TUKI (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.
Van Vallin, R. (2001). "Grammatical Relations in Ergative Languages". *Studies in Languages*, 5: 361-394.
Wesana-Chomi, E. (2003). *Kozi Tangulizi katika Sarufi Miundo ya Kiswahili*. Libya: Chuo Kikuu cha Sebha.